


# KIJASHO CHEMBAMBA

Na: Richard MWAMBE

©Jamvi la Simulizi 2025

## SEHEMU YA 4

### *Ilipoishia…*

*"Ndiyo yupo hapa, anasema usiogope uje ni jambo dogo tu!" yule mgambo akamwambia. Na simu ya Patel ikakatwa pasi na kutoa jibu lolote. Yule mgambo akajaribu kuipiga tena lakini haikuwa ikipokelewa kabisa. Dakika kumi baadae, Amata bado alikuwa eneo lile, liliwasili Land Cruiser jeusi na kuingia maegeshoni. Yule mgambo akamwambia Amata kuwa huyo aliyefika ni baba yake na Patel. Kweli, mlango ulipofunguliwa, waliteremka wanaume watatu. Wawili kati yao walikuwa watu wazima na mmoja alikuwa kijana kabisa. Walivuta hatua na kumfuata yule mgambo. Wakasalimiana.*

*"Yuko wapi bhana askari?" mmoja wao aliyeonekana mtu mzima aliyevalia kanzu aliuliza. Yule mgambo akawatambulisha kwa Amata. Wakasalimiana kisha wakamtaka Amata kuingia nao ndani ya lile jengo. Akawafuata.*

### *Endelea…*

Waliingia ndani ya ofisi yenye ukubwa wa wastani iliyokuwa na meza kubwa iliyosheheni makabrasha ya ofisi. Mbele ya meza ile kulikuwa na kiti kimoja na upande wa pili kulikuwa na makochi ya wageni. Katika makochi yale, Amata na wale wengine wawili akiwamo Patel waliketi. Patel alikuwa

mnyonge sana, aliyejawa wasiwasi na jasho jepesi lilionekana wazi kuanzia kwenye nywele zake.

"Bhana askari… wewe umwache mwanagu bhana, mengi bhanazungumzika," yule mzee akasema huku akivuta droo na kutoa vibunda vitatu vya noti na kuzitua mezani. Kwa hesabu ya harakaharaka ilikuwa kama Milioni tatu hivi shilingi za Kitanzania. Halafua akatoa vibunda vingine viwili akavitu mezani. "Hii ya kwako nah ii ya bosi yako, pelekea yeye mambo hii ikaisha," akasema. Amata alibaki akimtazama Mhindi yule, asimmalize.

"Hii pesa ni ya nini?" Amata akauliza.

"We ukapelekea bosi yako na familia yako… kijana wangu asiende huko," akaeleza.

"Asisende wapi?"

"Polisi!"

"Acheni kutoa rushwa ninyi watu, kumbe hii ni tabia yenu siyo? Kama mmetenda kosa na mnatakiwa kufika polisi ni lazima kufika polisi. Mnajua kwamba kutoa rushwa na kosa? Niwabebe wote muende wote kituoni?" Amata akaongea kwa ukali na mamlaka. Wakati Patel akitetemeka na kulowa jasho, baba yake alihisi haja kumtoka. Sumu ya Wahindi ni polisi. Amata aling'amua kuwa wanausalama wengi watakuwa wanatajirika kupitia wahindi hawa, kwa maana ukiwatia *jamba-jamba* tu wanatoa pesa. "Haya Patel yuko wapi?" Amata akauliza.

"Hiyo hapo bhana! Usipeleke yeye polisi, mimi nina toto bili tu…" yule mzee wa Kihindi akasema kwa kitetemeshi.

"Patel, hili duka ni la kwako?" Amata akauliza akimwangalia yule kijana.

"Ndiyo bhana…" yule kijana akajibu.

“Twende kuna kitu nahitaji kuona, ninyi subirini hapa…” Amata akawaambia wale wengine, kisha yeye na Patel wakaingia dukani.

Duka lilikuwa limesheheni vifaa vya elektroniki kama kompyuta mpakato, kamera na vinginevyo. Amata alisimama na kukagua kwa macho kila kilichopo humo ndani. Patel, yule kijana wa Kihindi alikuwa hajui hata kinachoendelea, alijawa na hofu na kubaki akitetemeka.

“Sikiliza Patel, leo mchana hapa palitoa ajali, ulikuwepo?” Amata akauliza kwa upole.

“Ndiyo bhana, mama moja gongwa vibaya na gari…” Patel akajibu.

“Enhe, sasa kilichonileta hapa ni kutaka kuona matukio hayo kwa kamera zako za usalama kwa kuanza na hiyo ya kwenye korido,” akamwambia. Patel alishusha pumzi ndefu na kujifuta jasho kwa kiganja cha mkono wake. Akavuta hatua na kuiendea runinga kubwa iliyopachikwa ukutani. Alipoiwasha, ilionesha maramoja matukio yaliyokuwa yakiendelea huko nje kupitia kamera kumi na sita tofauti. Patel alichagua kamera namba nane ambayo ilikuwa ikimulika sawia kwenye hiyo korido. Akarudisha muda mpaka alasiri ya siku ile. Amata aliweza kufuatilia tukio lote, aliweza kumuona Madam S tangu alipoanza kunaswa na ile kamera, mara akamuona akipigwa kikumbo na yule mtu na kusukumiwa barabarani.

“Hebu rudisha hapo…” akamwambia Patel. Yule kijana akafanya hivyo, “Simamisha…” akamwamuru. Patel akasimamisha mara yule mtu alipoonekana karibu na Madam S. “Ikuze hiyo picha!” akamwambia. Patel akaikuza na sura ya yule

mtu ikaonekana japo alikuwa amevaa miwani. "Nifanyie screenshot ya huyo mtu halafu naomba footage ya tukio," Amata akamwambia Patel. Kisha akachukua muda kutazama gari lililomgonga. Lakini aligundua kuwa halikuwa na namba ila tu ni Mazda.

Alipojiridhisha, akachukua vipande vyote vya zile picha kwenye kadi mmweko yake. Akamshukuru Patel na kumtaka asimwambie mtu yeyote juu ya hilo. Akaagana na wale wazee, akaondoka zake. Amata alidhamiria moyoni mwake kuanza na huyo mtu. *Ni nani?* Akajiuliza. Tayari damu ilimchemka, akili ilifanya kwa kasi ya mwanga. Nje ya duka lile, hakuondoka haraka, alivuka upande wa pili na kujificha pahala. Akahakikisha Patel na wale wazee wake wameondoka ndipo na yeye akaondoka zake.

✠ ✠ ✠

Ndani ya ofisi ya AGI Investment, katika jengo la JM Mall, Amata aliketi kwenye kiti chake kwa utulivu kabisa. Macho yake yalikuwa kwenye kioo cha kompyuta kubwa ya kisasa iliyo mbele yake. Tayari saa tano usiku ilikuwa ikiyoyoma kuelekea saa sita ya usiku. Kichwa cha Amata bado kilikuwa kikitafuta jambo ambalo wengine hawakuhangaika kulitafuta. Ndiyo alikuwa na majina kadhaa ambayo kwayo Madam S alihisi kuna hujuma iliyofanyia katika kuibwa au kutoweka kwa Kokwa ndani ya jumba la Makumbusho la Taifa. *Kokwa ni kitu hatari sana kuwa mikononi mwa mtu asiye na akili!* Aliwaza huku akiipakia ile video na picha kwenye kompyuta yake. Alipohakikisha kila kitu kipo sawa, akaipandisha ile picha kwenye mfumo maalum wa kiusalama unaoweza kutambua sura za watu na taarifa zao.

Amata aliruhusu picha ile ianze kuchunguzwa kwa ule mfumo wa kisasa zaidi. Ni Chiba wa Chiba aliyemuelekeza jinsi ya kuutumia kwa weledi. Sura nyingi za watu zilipita katika lile kioo, taarifa mbalimbali zilikuwa zikitembea kwenye kile kioo zikijaribu kuoana hapa na pale. Mfumo huu uliweza kuoanisha sura za watu kupitia uwiano wa kidevu, pua, macho ikiwamo na umbali wake ili kupata vipimo sahihi.

Dakika tatu na sekunde ishirini na moja zilitosha kumtambulisha Braison Sambala mbele ya macho ya Kamanda Amata. Mfumo ule ulimfananisha na mtu huyo kwa asilimia tisini na tano. Amata aliandika taarifa zake kwenye kitabu kidogo cha kumbukumbu. Ijapokuwa Amata alipata kumfahamu mtu huyo lakioni bado alihitaji uhakika zaidi kama ni yeye au la na jinsi gani ataweza kumpata kwa mahojiano. Saa sita na nusu usiku huo, Amata alitoka ofisini. Nje ya lile jengo akaingia kwenye moja ya magari yao ya ofisi ambalo lilikuwa hapo maegeshoni. Akaliwasha na kuondoka zake. Safari yake moja kwa moja iliishia katika ukumbi wa maofisa wa polisi Oysterbay. Hapo alikutana tena na Inspekta Simbeye.

"Vipi?" Simbeye alimuuliza kwa sauti ya chini iliyosongwa na kelele za muziki. Bendi ya Polisi Jazz ilikuwa ikitumbuiza usiku huo.

"Unamjua Braison Sambala?" Amata akauliza. Inspekta Simbeye alibaki kakodoa macho akimtazama Amata.

"We Braison umemjulia wapi?"

"Nijibu swali halafu tuendelee kuzungumza," Amata akamwambia Simbeye.

*♫ Karibu kwangu karibu, mchumba wangu Edina oooh*
*Wala usiwe na wasiwasi, mimi bado sijaoa oooh*
*Usirudie mlangoni tu, hapa ni kwako karibu…♫*

Mashairi ya wimbo uliokuwa ukipigwa na Polisi Jazz ulitawala ukimya wa watu hawa wawili waliokuwa wakitazamana kama majogoo yanayotaka kupigana.

"Braison Sambala ni jambazi sugu, jeshi la polisi tunamtafuta kwa udi na uvumba… una shida naye gani?" Simbeye akauliza.

"Katika uchunguzi wangu wa awali kuhusu ajali ya Madam S, Braison anahusika…" Amata akaeleza.

"Kivipi?"

Amata akamwonesha ile video clip kupitia kifaa chake maalumu. Simbeye akatikisa kichwa juu chini, "Huyu mshenzi yupo mjini hapa?" akauliza.

"Kama unajua anapopatikana namuhitaji haraka iwezekanavyo, kupitia yeye nitajua chanzo cha ajali ya HOT…" Amata akaeleza.

"Huyu ni jambazi tunayemtafuta sana, ukimpata utakuwa umetusaidia mno," Simbeye akamwambia Amata. Saa saba usiku ilikuwa ikiyoyoma, watu walipungua taratibu katika bwalo lile na kubaki wachache walioendelea kuburudika na muziki.

"Kaman nyie wengi mmemkosa mimi mmoja nitampataje?" akauliza huku akiitazama saa yake.

"Anyway… umemuona mama yako?" Simbeye akauliza.

"Hapana, sihitaji kumuona kama sina taarifa nzuri mkononi mwangu," Amata akajibu na kuagana na Amata. Ulikuwa usiku mnene, usiku wa wezi na wachawi, wanga na walozi,

machangudoa na wazurulaji, zaidi yao ni wanausalama wanaopiga doria. Amata aliwasha gari lake na kuondoka eneo lile. Moja kwa moja alifika Msasani nyuma ya Mayfair Plaza. Katika majumba makubwa ambayo yalijengwa huko nyuma karibu na bahari, mojawapo lilikuwa likimilikiwa na Gina. Jumba kubwa la kisasa, Gina alikuwa akiishi na wadogo zake wawili ambao mara nyingi walikuja tu wakati wa likizo. Usiku wake aliupitisha pale japo Gina mwenyewe hakuwapo.

✠ ✠ ✠

Asubuhi mapema, siku iliyofuata, Amata akiwa na Marcedec Benz, mali ya jasusi la kike, Gina, aliwasili Mtaa wa Milambo. Lengo la kwenda katika mtaa huo ni kuendelea na upelelezi wake juu ya vipi atampata Braison Sambala. Katika kazi yake siku zote hakuwahi kuuchunguza mtaa wa Mirambo kwa kuwa haukuwahi kuwa na matukio ya kumfanya kuwa hapo. Aliuchunguza harakaharaka na alipojiridhisha kile akachokitafuta. Aliondoka kuelekea kituo kikuu cha polisi kilichopo karibu na makutano ya Barabara ya Sokoine na Gerezani.

“Karibu! Tukuhudumie nini?” sauti isiyo na chembe ya ukarimu ya askari mmoja wa usalama barabarani aliyekuwa nyuma ya dawati la mapokezi ilimfikia Amata. Amata akaonesha kitambulisho chake cha upolisi, akapewa heshima zote na huyo bwana.

“Nahitaji kuwaona watu wa kamera za barabarani,” akamwambia. Yule askari akamwongoza mpaka kwenye chumba maalum ambapo alikutana na mkuu wa kitengo hicho. Akaeleza shida yake na hakukuwa na tatizo mara baada ya kuonesha utambulisho wake bandia.

Katika chumba hicho palikuwa na askari vijana wanne watatu wanaume na mmoja wa kike. Amata alipokelewa na kupewa kiti. Kwa kuwa taarifa ilishafika kutoka kwa mkuu wa kitengo, walikuwa tayari kumhudumia. Walimtambua kama Mrakibu Msaidizi wa Polisi ASP kwa nyota zake tatu za bandia.

"Nahitaji kuona footage ya camera ya jana saa nane na robo hivi, magari yanayotoka Mtaa wa Mirambo na kuingia Barabara ya Samora kuelekea Ikulu," akawaambia. Yule mwanadada, maramoja, akaivuta hiyo kamera na kusogeza muda mpaka kuupata huo uliotajwa. Dakika mbili hivi, Amata aliweza kuling'amua lile gari, likiingia kwa kasi katika ile barabara, "Fuatilia hilo gari mpaka linapoishia," akamwambia. Yule mwanadada akafanya hivyo na kulifuatilia lile gari mpaka lilipoacha barabara ya Sokoine na kukunja kushoto Mtaa wa Shabban Robert. Jambo ambalo Amata hakuamini ni kwamba lile gari liliishia kwenye Ofisi Ndogo za Bunge. "Hebu rudia…" akaomba maana alihisi wazi kuwa haamini anachokiona. Lakini tukio lilikuwa lilelile. Amata akaomba apewe kipande cha footage ile. Baada ya kukidhi vigezo vyote alipewa nakala ile ya dakika nne tu. Amata akaondoka zake. *Tunahujumiana hapahapa!* Kamanda Amata aliwaza maana aliona kama lile gari liliingia hapo Ofisi ndogo ya Bunge maana yake mmiliki aweza kuwa mtu wa serikali tena mwenye wadhifa wa juu. Kutoka Ofisi ndogo za Bunge mpaka Ofisi Ndogo ya TSA ni mwendo wa mguu usiozidi hata dakika tano. "Anatujua vizuri!" akajikuta kasema kwa sauti. Akaicha Barabara ya Sokoine na kukunja ile ya Shabban Robert, akapita kwenye lango la Ofisi ndogo za Bunge na kuliona lile gari likiwa kwenye maegesho. Akapita moja kwa moja na kuchukua Barabara ya Luthuli mpaka jengo la Hazina zilipo ofizi ndogo za

TSA. Akaingiza gari ndani na kuliegesha. Akazima injini na kutulia kimya bila kushuka.

"Sasa kazi inaanza!" akajisemea na kuchukua bastola kutoka kwenye lile gari, akaikagua na kuhakikisha ipo sawa. Akafyatua kitasa cha mlango, akateremka na kulirudia lango. Sasa kamanda Amata alikuwa akiongozwa na hasira zaidi kuliko utashi. Akatoka nje ya uzio na kuvuta hatua kuelekea Ofisi ndogo za Bunge. Lengo lilikuwa ni kumtaka mmiliki wa hilo gari na nani alikuwa akiendesha. Aliamini kuwa hao wangeweza kumfanya ampate Braison Sambala. Na kupitia wao angeweza kuanza kuingia ndani ya hujuma na kugundua tatizo. *Je wanahusika na upotevu wa Kokwa au kuna jingine?* Akajiuliza.

Kwa maoni tuandikie

**Whatsapp 0766974865**